

JinaNambari yako:.....

Tarehe:.....Sahihi:.....

102/2
KISWAHILI
LUGHA
JUNI 2016
MUDA: SAA 2 ½

**MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA MARAFIKI
KAUNTI NDOGO YA KAKAMEGA MASHARIKI-2016**

102/2
KISWAHILI
LUGHA

Andika jina lako, nambari , terehe na sahihi katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

Jibu maswali yote. Majibu yako yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA		

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kasha ujibu maswali

Ilikuwa Jumamosi. Nilifika nyumbani kwangu saa moja jioni. Tangu nistaafu miaka miwili awali sikupenda kuchelewa Taarifa ya Habari.

Mwezi mmoja ukawa umepita tangu nipewe pesa za **kiinua mgongo**. Mwezi mmoja mzima nilikuwa katika shughuli za kulipa deni hapa na kulipa karo huku. Kuwekeza kwenye mradi ule na kununua hili. Sasa shilingi laki mbili tu zilikuwa zimesalia katika benki.

Watu wengi walinshawishi nijaribu kilimo cha mahindi. Bei ilikuwa imeanza kuimarika. Katika taarifa ya habari jioni hiyo, Waziri wa kilimo alitangazaa bei mpya , shilingi 1,500 kwa kila gunia. Nami nilikuwa naanza kuumakinikia mradi huu.

Baada ya taarifa, nilioga nikala na nikaenda kulala. Kwa sababu ya uchovu, usingizi ulinichukuwa mara moja. Usingizini niliota. Katika ndoto niliutekeleza mradi wangu. Msimu huo wa kulima nilitenga hekari kumi za shamba langu. Wataalamu walinishauri kuwa wakati mzuri wa kulima ni wa kiangazi. Mwezi wa Januari ulipoanza tu nilitafuta trekta na kulima. Malipo yalikuwa shilingi 1,200 kila ekari. Katikati ya mwezi wa Mechi, nilitafuta trekta la kutifua shamba tena kwa gharama ya shilingi 15,000 ekari zote kumi. Kufuatia ushauri wa **manyakanga wa kilimo**, nililipa shilingi elfu kumi na tatu kupiga shamba lote haro.

Mwishoni mwa mwezi huo, nilienda mjini kutafuta pembejeo. Kwanza, nililipa shilingi 20,500 kwa magunia 15 ya mbolea. Kisha nilinunua magunia manne ya mbegu ya mahindi yenye uzani wa kilo 25 kwa shilingi 3,300 kila gunia. Mwezi wa Aprili ulipotimia tu, niliamua kupanda ili nipate mazao bora, nilipanda kwa tandazi. Gharama ilikuwa shilingi 1,000 kila ekari. Mvua ilinyesha vizuri na baada ya siku saba, mahindi yalianza kuota. Ilifurahisha kuhesabu mistari ya kijani iliyonyooka. Hali hii iliwezekana tu baada ya kuajiri vijana wa kuwafukuza korongo na vidiri ili wasifukue mbegu mchangani.

Baada ya mwezi mmoja, hatua ya kupalilia ilifika. Nilitafuta vibarua wa kupalilia. Malipo yalikuwa shilingi 700 kila ekari. Kumbe kupalilia kulichochea mtifuko wa mahindi. Punde yakawa yanarifika magotini. Hii ikawa ishara kuwa yanahitaji kumwagiwa mbolea ya kunawirisha iitwayo 'amonia'. Gharama yake ikawa shilingi 1,300 kila gunia. Hivyo , nikalipa shilingi 19,500 kwa magunia kumi na matano.

Mahindi yalibadilika kimiujiza. Ghafla tu yalirefuka na kunenepa mashina. Yalibadilika rangi yakapiga weusi. Shamba liligeuka likawa kama msitu wa rangi ya kijani iliyokolea. Wapita njia walijababika mimea na juhudi zangu. Shamba langu sasa likawa kielelezo. Maafisa wa kilimo wakawa kila siku wanawaleta wakulima wengine kujifunza siri ya ufanisi wangu. Hapo nikaanza kuhesabu mavuno nitakayopata na kukadiri faida. Nilipuuza kabisa ushauri wa wahenga kuwa **'Usikate majani, mnyama hajauawa.'**

Bila taarifa wala tahadhari mvua ilitoweka. Hayakupita majuma mawili mahindi yakaanza kubadilika. Juma moja baadaye mahindi yalinyauka. Badala ya mahindi, shamba likageuka la vitunguu vilivyochomwa na jua. Makisio yangu ya faida yaliyeyuka jinsi ufanyavyo moshi.

Lakini ‘Muumba ndiye Muumbua.’Siku moja mawingu yalitanda na mvua ikanyesha , muda si muda mahindi yalianza kunawiri. Kumbe tukio lililowavunja moyo lilikuwa laja. Siku moja mvua kubwa ilinyesha. Asubuhi nilipotoka nje nilipigwa na butwa. Barafu ilitapakaa pote. Shamba lilikuwa limetapakaa barafu nafuu. Nilipotazama upande wa shamba niliona dalili za majani mapya ya mahindi yakianza kuchomoza. Maumbile ni kitu cha ajabu kweli.

Muda si mrefu mahindi yalirudia hali yake tena, kasha yakakomaa. Harakati za kutafuta watu wa kuyakata na kuyakusanya zilianza. Gharama ya shughuli hii ikawa shilingi 5,000 kuvuna kusafirisha kutoka shamba na kukoboa kwa mashine magunia 200 yakachukua shilingi 20,500. Kufikia hapo nilikuwa nimetumia takribani shilingi 192,700. Gharama nyingine zilikuwa za usafiri, gharama ya dharura na usimamizi, usumbufu wangu binafsi, gharama ya magunia na kadhalika. Mahindi yalipokuwa tayari kwenye magunia nilifunga safari kwenda mjini kutafuta soko. Niliposhuka tu niliona gazeti. Habari motomoto siku hiyo ilikuwa ‘MAHINDI GUNIA 900/=’ Niligutuka usingizini.

MASWALI

a) Ni changamoto zipi zinazokumba kilimo. (al.4)

.....
.....
.....
.....
.....

b) Msimulizi alikuwa na kiasi gani cha pesa katika benki baada ya mradi kukamilika? (al.2)

.....
.....

c) Eleza maana ya methali zifuatazo kwa mujibu wa makala.

i. Usikate majani, mnyama hajauawa. (al.1)

.....
.....

ii. Muumba ndiye Muumba. (al.1)

.....
.....

d) Eleza mambo mawili yaliyosababisha msimulizi asipate faida alivyotarajia. (al.4)

.....
.....
.....

e) Kwa nini msimulizi alisema maumbile ni kitu cha ajabu? (al.1)

.....
.....

f) Eleza maana ya:

i. Kiinua mgongo (al.1)

.....
.....

ii. Manyakanga wa kilimo. (al.1)

.....
.....

2. UFUPISHO: (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.

Katika ulimwengu huu tunaishi wenye hekaheka nyingi, mwanadamu anaendeshwa na maisha mfano wa gurudumu la gari. Kwa watu wenye kufanya kazi katika mazingira ya ofisi ambapo wanaketi mchana kutwa, mazoezi ni muhimu sana. Baadhi ya watu huona fahari wapigapo tai na kuelekea au kutoka kazini kwa gari. Tabia hii ya mwanadamu inamsahaulisha kuwa mwili wake ulidhamiriwa kufanya mazoezi ya viungo kwa kutembea au kufanya kazi zenye kuhitaji misuli kuoashwa moto. Watu wengi hawana habari kuwa mazoezi yana faida tele kwao.

Wataalamu wa sayansi wamebainisha kuwa watu wanaoidhiki miili yao kwa mazoezi ya mara kwa mara huishi zaidi kuliko wasiofanya mazoezi. Watu hawa huwa wamo katika hali nzuri ya afya na wenye nguvu kuliko wale ambao hawaishughulishi miili yao kwa mazoezi au kazi zinazohitaji utumiaji nguvu.

Ni dhahiri kwamba mazoezi huchochea kuundwa kwa seli mpya za ubongo. Utafiti wa kisayansi umebainisha kuwa sehemu za ubongo zenye kusisimuliwa kwa mazoezi ndizo hutekeleza jukumu la kukumbuka na kujifunza. Bila mazoezi sehemu hizi zitashindwa kukumbuka au kujifunza maarifa mapya. Vile vile, imethibitishwa kwamba watu wanaoshiriki shughuli zenye kuwahitaji kutumia nguvu hutia fora katika mambo yanayowahitaji kukumbuka, kufanya maamuzi, pamoja na kusuluhisha matatizo.

Hali kadhalika, mazoezi huimarisha siha ya binadamu. Mathalani, matatizo ya moyo yanaweza kukabiliwa kwa kufanya mazoezi ya viungo. Kufanya mazoezi mara kwa mara huufanya moyo kuwa imara na kuuwezesha kutekeleza jukumu lake ipasavyo. Ifahamike kwamba moyo wenye siha huweza kupiga kiasi kikubwa cha damu bila ya juhudi kubwa. Hili bila shaka litamkinga binadamu dhidi ya kulemewa na kazi.

Isitoshe, kushiriki mazoezi au shughuli zenye kutumia nguvu mara kwa mara huweka mwili katika hali nzuri ya kupambana na magonjwa. Utafiti wa kisayansi umeonyesha kuwa shughuli kiasi zinazomhitaji mtu kutumia nguvu, pamoja na upunguzaji wa uzito, na uzingatiji wa lishe bora, huweza kupunguza uwezekano wa kupata ugonjwa wa kisukari kwa baina ya asilimia 50 na 60. Mazoezi hayapunguzi tu shinikizo la damu, bali pia hatari ya kupata kiharusi. Aidha, kufanya mazoezi mara kwa mara husaidia kuthibiti uzani wa mwili. Mtu anapokula kiasi cha chakula kinachozidi mahitaji yake ya kimwili huweza kujinenepea na kushindwa kutekeleza majukumu ya kimsingi. Mazoezi husaidia kuzichoma kalori zisizohitajika mwilini. Hatua hii, licha ya kusaidia kupunguza uzani, huvisisimua viungo vya mwili. Matokeo ya haya ni utendakazi wa hali ya juu bila kuchoka. Vilevile mwili unaofanya mazoezi haudorori. Umbo la mtu anayefanya mazoezi hupendeza.

Juu ya hayo, kufanya mazoezi mara kwa mara husaidia kujenga misuli yenye nguvu. Misuli inapokuwa na nguvu tunaweza kulifanya jambo kwa muda mrefu bila kuchoka. Mbali na misuli kuimarika, mazoezi na shughuli zinazohitaji utumiaji nguvu husukuma hewa na virutubisho kwenye viungo mahususi vya mwili na kuvisaidia kufanya kazi vyema zaidi.

Hali kadhalika mazoezi husaidia kujenga mifupa. Kadri binadamu anavyoshiriki katika shughuli kama vile kuruka, ndivyo anavyoimarisha mifupa yake. Shughuli ya aina hii huipa mifupa uzito ambao unaiwezesha kukua na kujengeka ikiwa na nguvu. Mazoezi pia hukawiza kudhoofika kwa mifupa.

Kunyooshanyoosha viungo nako huchangia kuufanya mwili kuwa imara na wenye kunyumbuka. Hali hii ya mwili hupunguza uwezekano wa kupata majeraha. Mwili usionyumbuka humfanya mtu ashindwe kutekeleza hata shughuli nyepesi zinazomhitaji

.....
.....
.....
.....
.....
.....

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) i) Eleza maana ya Kirai. (al.2)

.....
.....

ii) Tambua aina za virai vilivyopigiliwa mstari katika sentensi ifuatayo. (al.1)

Jirani mwema alinipa chakula.

.....
.....

b) Bainisha aina ya chagizo katika sentensi ifuatayo:

Barabara za mjini zimetengenezwa upya. (al.1)

c) Onyesha viambishi awali na tamati katika kitenzi:

Alimchezea. (al.2)

d) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya **karama** na **gharama**. (al.2)

.....
.....

e) Onyesha **Kiima** na **Shamirisho** katika sentensi ifuatayo:

Maria alimbebea mwalimu mzigo kwa gari. (al.2)

f) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali. (al.3)
Mama alifika tulipokuwa tukilima.

g) Kwa kutoa mifano mwafaka, eleza aina za sentensi zifuatazo:-

i. Sentensi ya masharti. (al.2)

.....
.....
.....

ii. Sentensi tata. (al.2)

.....
.....
.....

h) i) Eleza maana ya mofimu. (al.1)

.....
.....

ii) Bainisha mofimu katika neno:

atamnywea (al.3)

i) Tunga sentensi mojamboja kubainisha:-

i. Kihusishi cha wakati. (al.1)

.....
.....

ii. Kihusishi cha ulinganisho. (al.1)

.....
.....

iii. Kitenzi kishirikishi kipungufu. (al.1)

.....
.....

iv. Kiunganishi cha kinyume. (al.1)

.....
.....

j) Tunga sentensi tatu kudhihirisha matumizi matatu ya mshazari. (al.3)

.....
.....
.....
.....

k) Andika sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali timilifu. (al.2)

Yohana huwapigia watu nguo pasi.

.....
.....

l) Tunga sentensi kutumia kitenzi fa katika kauli tendwa. (al.1)

.....
.....

m) Tumia 'kwa' katika sentensi kuonyesha.(al.2)

i. Sababu

.....
.....

ii. Pamoja na

.....
.....
n) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo. (al.1)

Madebe hayo yatasafirishwa pamoja na nyundo hizi.

.....
.....
o) Andika sentesni ifuatayo katika hali yakinishi. (al.1)

Usingeacha masomo, usingetaabika vile.

.....
.....
p) Taja na utofautishe vipasuo vya ufizi. (al.2)

q) Eleza maana mbili za sentensi. (al.2)

Yohana alimpigia Juma mpira.

.....
.....
.....
.....
r) Andika katika msemu wa taarifa “Nitakuarifu nikimwona”, Maria alisema. (al.1)

.....
.....
4. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

a) Eleza maana ya viziada lugha. (al.2)

.....
.....
.....
.....
b) Toa sababu **tatu** zinazofanya watu watumie viziada lugha. (al.3)

.....
.....
.....
.....

c) Ni siku ya wazazi shuleni mwenu. Umechaguliwa kutoa hotuba siku hii. Eleza sifa **tano** za lugha utakayotumia. (al.5)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....